



Changamoto za Kuhifadhi Lugha ya Kiswahili Katika Zama za Utandawazi

Jalgham Abuazuom Emhemmed Ali

Department of African Languages and Studies, Faculty of Languages, Sebha Universty, Libya

Maneno muhimu :

Changamoto
Elimu
Teknolojia
Utandawazi
zama

MUHTASARI:

Utafiti huu unachunguza changamoto zinazolikabili lugha ya Kiswahili katika zama za utandawazi, ambapo maendeleo ya kijamii, kiutamaduni na kiteknolojia yameathiri pakubwa matumizi na hadhi ya Kiswahili. Lugha za kigeni kama Kiingereza na Kifaransa zimepewa kipaumbele katika sekta za elimu, biashara na teknolojia, hali inayosababisha Kiswahili kupoteza nafasi yake ya hadhi. Changamoto nyingine ni uhaba wa rasilimali za lugha, ikiwemo kamusi, vitabu vya kitaaluma na maandiko ya kidijitali, jambo linalodumaza maendeleo ya kitaaluma na kitaifa ya Kiswahili. Utafiti umetumia mbinu ya kimaelezo (descriptive method) na kuongozwa na nadharia ya soshilinguistiki, ili kuchunguza uhusiano kati ya lugha na muktadha wa kijamii na kimataifa. Data zimekusanywa kupitia uchambuzi wa maandiko, makala za kitaaluma, mahojiano na hojaji, hatua iliyowezesha kupatikana kwa mtazamo mpana na wa kina kuhusu changamoto zinazolikabili Kiswahili. Matokeo yanaonyesha kuwa bila jitihada za makusudi kutoka kwa serikali, vyombo vya habari na jamii, Kiswahili kiko katika hatari ya kudhoofika zaidi. Hivyo, kuna haja ya mikakati ya pamoja ya kukilinda, kukiendeleza na kukipa nafasi pana kama lugha ya taifa na pia lugha ya kimataifa.

تحديات الحفاظ على اللغة السواحيلية في عصر العولمة

جلغم ابوعزوم امحمد علي

قسم اللغات والدراسات الأفريقية ، كلية اللغات ، جامعة سبها ، ليبيا

الملخص	الكلمات المفتاحية:
يتناول هذا البحث التحديات التي تواجه اللغة السواحيلية في ظل العولمة، حيث أثرت التحولات الاجتماعية والثقافية والتكنولوجية تأثيراً كبيراً على استعمالها ومكانتها. فقد أصبحت اللغات الأجنبية مثل الإنجليزية والفرنسية تحظى بالأولوية في مجالات التعليم والتجارة والتكنولوجيا، مما أدى إلى تراجع مكانة اللغة السواحيلية. ومن التحديات الأخرى نقص الموارد اللغوية مثل القواميس والكتب الأكاديمية والنصوص الرقمية، الأمر الذي يعيق نمو اللغة وتطورها في المجالات الأكاديمية والمجتمعية. وقد اعتمدت هذه الدراسة على المنهج الوصفي واستندت إلى النظرية السوسiolسانية، وذلك بغرض تحليل علاقة اللغة بسياقها الاجتماعي والدولي. أما أدوات جمع البيانات فقد شملت تحليل الوثائق والمراجع الأكاديمية، والمقالات العلمية، بالإضافة إلى المقابلات والاستبيانات، مما أتاح فهماً أوسع وأعمق للتحديات التي تعترض اللغة السواحيلية. وتظهر النتائج أنه في غياب جهود جادة من قبل الحكومات ووسائل الإعلام والمجتمع، تبقى اللغة السواحيلية مهددة بمزيد من التراجع. وعليه، تبرز الحاجة إلى وضع استراتيجيات مشتركة للحفاظ عليها، وتطويرها، وتعزيز مكانتها بوصفها لغة وطنية وإقليمية وعالمية.	العولمة التحديات التكنولوجيا عصر العلم

Utangulizi:

Lugha ya Kiswahili ni mojawapo ya lugha zilizo katika hatari ya kupoteza uasili wake na hata kudidimia miongoni mwa wazawa wake pamoja na wazungumzaji wa kigeni kutoka janibu mbalimbali. Kuhifadhiwa kwa lugha hii ashirafu kumekuwa suluhu kubwa la kuzuia maangamizi yake mikononi mwa waja wasiojali lolote kuhusu makuzi ya lugha hii. Hali kadhalika, uhifadhi wa lugha ya Kiswahili umeathirika pakubwa na suala la utandawazi. Je, utandawazi ni nini? Kulingana na Kamusi ya Kiswahili Sanifu (2018, Uk.704), utandawazi

ni mfumo wa uhusiano wa kimataifa katika sekta mbalimbali zikiwemo uchumi, biashara au siasa uliofanikishwa na kuimarika kwa teknolojia ya habari inayosababisha uepesi wa mawasiliano baina ya mataifa na jamii mbalimbali. Licha ya faida na mafanikio mengi yanayotokana na uhifadhi wa lugha ya Kiswahili katika zama hizi za utandawazi, kuna changamoto tele ambazo zinahusishwa na uhifadhi wa lugha hii. Miongoni mwa changamoto hizi ni pamoja na mabadiliko ya teknolojia, sera mbovui za elimu, upungufu wa

*Corresponding author:

E-mail addresses: jal.ali@suj.sebhau.edu.ly

Article History : Received 22 July 2025 - Received in revised form 20 September 2025 - Accepted 30 September 2025

raslimali, mabadiliko ya tamaduni, upungufu wa uhamasishaji, na ushindani wa lugha za kigeni (Matundra, 2019). Hivyo basi, makala haya yanadafua kwa kina uhifadhi wa lugha ya Kiswahili kwa kujikita sana katika changamoto za kuhifadhi lugha hii katika zama za utandawazi.

Maswali ya utafiti

1. Je, maendeleo ya kijamii, kiutamaduni na kiteknolojia yameathiri vipi hadi na matumizi ya Kiswahili?
2. Kwa nini lugha za kigeni zimepewa kipaumbele katika elimu na biashara, na ni kwa namna gani hili limeathiri Kiswahili?
3. Je, uhaba wa rasilimali za Kiswahili (kamusi, vitabu vya kitaaluma na maandiko ya kidijitali) unachangia vipi kudorora kwa Kiswahili?

Kuhifadhi Lugha ya Kiswahili Katika Zama za Utandawazi:

Utandawazi umechukuwa nafasi pana katika kufanikisha uhifadhi wa lugha ya Kiswahili. Watafiti kadha na kadha nyanjani wamebaini kwamba kila lugha ipo katika hatari ya kuathirika kwa kushindwa kuhimili nguvu za mabadiliko ya kiuchumi, ukandamizaji wa kielimu, nguvu za kivita na mihimili ya kidini. Wanajopo wa utafiti katika shirika la UNESCO pia wamebaini kwamba uhifadhi wa lugha ya Kiswahili unaweza kabiliwa na mtazamo hasi miongoni mwa watumiaji wa lugha hiyo. Aidha, inasemekana kwamba utandawazi unaotukiza lugha za kigeni una athari kubwa katika makuzi, maenezi, na uhifadhi wa lugha ya Kiswahili katika ukanda wa Afrika na sehemu nyingi duniani (Mazrui & Mazrui, 1995). Kiswahili kimesalia kuwa amali adimu kwa mawasiliano na utambulisho wa jamii yake, jinsi yalivyo majukumu ya lugha zingine duniani. Hii sababu ndiyo lengo murua la kuhifadhi na kuchapuzi makuzi ya lugha ya Kiswahili ili iweze kudumu na kurithishwa kwa vizazi vya usoni.

Zama hizi za utandawazi zimefanikisha kuwepo kwa njia ainati za kuhifadhi lugha ya Kiswahili Afrika na dunia nzima. Mifano, kubuni sera madhubuti zinazozunguka matumizi ya lugha ya Kiswahili husaidia kwa kuzielekeza hatua za kupanga na kuindeleza lugha kama njia mojawapo ya kuhifadhi katika ukale wake. Kuhifadhi kwa lugha hii pia ni kupitia amri katika baadhi ya mataifa barani Afrika kama vile Kenya na Tanzania kuvfundisha Kiswahili kama somo la lazima ili kusaidia kuendelea kuwepo kwa lugha hiyo. Hii ni hatua murua ya kuhifadhi Kiswahili. Utafiti wa miradi kupitia miungano kama vile Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (TUKI), Chama Cha Kiswahili Afrika (CHAKA) na Chama Cha Kiswahili Duniani (CHAKIDU) imekuwa njia mahususi ya kuhifadhi lugha ya Kiswahili. Hali kadhalika, maandalizi mema ya wakufunzi na wataalamu katika nyanja mbalimbali za Kiswahili ni shinikizo mufti linalotumika kama hifadhi adimu ya lugha ya Kiswahili (Mulokozi, 2004). Serikali nyingi duniani pia zimefadhili uchapishaji na urudufu wa Makala na vitabu mbalimbali vinavyohusu mawanda ya lugha ya Kiswahili kama njia mojawapo ya kuhifadhi lugha ya Kiswahili. Shughuli za maeneo rasmi kama vile bunge za Kenya na Tanzania, shughuli za kidini, siasa na elimu zimesisitiza matumizi ya lugha ya Kiswahili kama njia ya mawasiliano, hivyo kuwezesha uhifadhi wa lugha hii kupitia vinywa na bongo za wahusika pamoja na vyombo vya kielektroniki vinavyoambatanishwa kurekodi na kupaza sauti. Utafsiri wa nyaraka mbalimbali zinazohifadhiwa makashani na matumizi ya vyombo vya habari ni hifadhi kamili ya lugha ya Kiswahili miongoni mwa watumizi na watunzi wake (Ndung'u na wenzake, 2022). Vilevile, shughuli za sana na maonyesho zimejikita katika matumizi ya lugha ya Kiswahili kwa hivyo kuipa hifadhi kubwa miongoni mwa hadhira tendi pamoja na tuli wakati wa mawasilisho ya sanaa hizo.

Changamoto za Kuhifadhi Lugha ya Kiswahili Katika Zama za Utandawazi:

Watafiti wengi na wanaharakati wa kukitetea, kukikiza na kukihifadhi Kiswahili kama mojawapo ya lugha na amali ya wanajamii wamekumbana na changamoto ainati. Mchakato huu umekumbwa na balaa si haba zinazotatiza na kujaribu kukandamiza uhifadhi na makuzi ya lugha ya Kiswahili. Miongoni mwa changamoto hizi ni kama vile ushindani wa lugha za kigeni, upungufu wa rasilimali, mabadiliko ya tamaduni, sera mbovu za elimu, kukosekana kwa uhamasishaji, mabadiliko ya teknolojia, uchache wa watafiti, mitazamo hasi ya jamii mbalimbali na hamahama za watu.

Ushindani wa Lugha za Kigeni:

Athari ya lugha za kigeni katika lugha ya Kiswahili ni mojawapo ya vipengele muhimu vinavyopaswa kuzingatiwa katika mijadala inayohusu changamoto za kuhifadhi lugha ya Kiswahili. Mintarafu ya tahariri ya Matundura (2019) katika gazeti la Taifa Leo, lugha za

kigeni kutoka nje ya bara la Afrika zimeathiri pakubwa makuzi, maenezi na uhifadhi wa lugha ya Kiswahili. Matundura anazidi kueleza katika makala yake kwamba wageni kutoka nje ya bara la Afrika wanaojikita kwenye mfumo wa utandawazi wameathiri uzingatifu na uhifadhi wa lugha ya Kiswahili. Makala ya Matundra pia yanafanua kwamba hizi athari hususan huwa za kimsamiati au za kileksikoni. Waarabu, Waajemi, Wamisri na Wachina ni miongoni mwa wageni wa awali waliozuru pwanu ya ukanda wa Afrika Mashariki. Watafiti wa historia chimbo wamethibitisha kuwepo kwa maandishi ya Wamisri na vyungu vya Wachina kama ishara tosha ya kuzuru kwa wageni katika ukanda huo mapema miaka ya 900 baada ya ujio wa Kristo (Batibo, 2005) Ujio wa lugha hizi tangu zamani umekuwa tisho kwa makuzi na maenzi ya lugha ya Kiswahili. Baadhi ya kazi za utafiti wa kiakiojia huonelewa bora kuhifadhiwa katika lugha za wahusika asilia, kwa hivyo kukinyima Kiswahili majukumu ya kuhifadhi habari hizo, basi kulifanya changamoto katika uhifadhi wa lugha ya Kiswahili.

Lugha zingine ambazo zimeshamiri katika enzi za utandawazi ni pamoja na Kiingereza, Kifaransa na Kilatino. Utandawazi umechangia kuenea kwa lugha hizi kwa kasi kama moto nyikani kupitia taasisi mbalimbali kama vile dini, elimu, siasa na taasisi za kiuchumi. Kupitia elimu, Kiingereza kimepewa kipaumbele miongoni mwa vitengo vyote vya shule hususan ukanda wa Afrika na maeneo mengi duniani (Kioko, 2013). Masomo mengi huendeshwa katika lugha ya Kiingereza na Kiarabu katika mataifa ya Afrika. Hii sababu hukipa Kiswahili nafasi finyu ya kujiendeleza, kukua na kuhifadhiwa miongoni mwa watumizi wake ikilinganishwa na lugha zingine. Hali kadhalika, ushindani mwingine baina ya lugha ya Kiswahili na luha zingine unajitokeza pale ambapo lugha zingine kama vile Kiingereza, Kiarabu, na Kifaransa zimepewa hadhi ya juu ikilinganishwa na Kiswahili. Matumizi ya lugha mbalimbali yamejenga utabaka kiasi kwamba watumizi wa lugha za kigeni kama vile Kiingereza na Kifaransa wanaonelewa kama watu wa tabaka la juu au wenye hadhi pevu ikilinganishwa na watumizi wa Kiswahili na lugha zingine za Kiasili (Abdulaziz, 1989). Hili swala huibua ushindani mkali wa nafasi ya kuenea na kuhifadhiwa baina ya Kiswahili na lugha zingine.

Upungufu wa Raslimali:

Raslimali ni kigezo mahususi cha taifa, jamii, eneo au mtu binafsi cha kuzingatia katika utekelezaji wa majukumu mbalimbali. Shughuli zozote zinazohusika na uhifadhi na makuzi ya lugha ya Kiswahili huhitaji angalau msukumo wa kifedha ili kurahisisha shughuli hizo. Kwa mfano, uhifadhi wa lugha ya Kiswahili angalau huhitaji wajuji wenye tajriba ya kiwango fulani, vifaa mahususi, muda wa kutosha na ujuzi au ufundi unaoendana na mifumo ya utandawazi na ya kisasa. Mataifa mengi ndani na nje ya Afrika yametenga raslimali finyu sana za kusaidia katika uchunguizi na uhifadhi wa lugha ya Kiswahili. Hili huenda ikawa ni kwa ajili ya sababu kadha wa kadha zikiwemo kuenea lugha zingine fahari kulinganishwa na lugha ya Kiswahili (Ndung'u na wenzake, 2022). Kwa hivyo mataifa kama hayo huona ni hasara au kukosa kuwajibika raslimali zinapotengewa shughuli kama hizo.

Watunzi au walinzi wa lugha ya Kiswahili ni watumizi wa lugha yenyewe. Watunzi hawa haswa kulingana na mifumo ya kisasa ya mtagusano baina ya watu, ni wazi kuwa wanahitaji kisomo na kiwango fulani cha kiufundi ili kufanikisha jambo hili kwa wepesi. Uchehefu wa fedha na raslimali zingine zinazohitajika katika kusoma au kupokea ujuzi wa kipekee ili kusaidia kuimarisha mbinu za kutunza na kuhifadhi lugha ya Kiswahili huzua changamoto kufanya shughuli hiyo kutatizika (Abdulaziz, 1989). Uhifadhi wa lugha ya Kiswahili na utekelezaji wa shughuli zozote zinazohusika na makuzi ya lugha hii huhitaji angalau vifaa vya kisasa ili kuwezesha uhifadhi wake katika zama hizi za utandawazi. Mashine ya kielektroniki kama vile tarakilishi, rekoda, kamera zinazohusika katika kuhifadhi wa lugha ya Kiswahili pia zina gharama ya juu ambayo watafiti na wataalamu wanaohusika na kuhifadhi lugha hii hupata wakati mgumu kwa sababu ya upungufu wa fedha. Vifaa hivi kwa wingi pia huhitaji nguvu za umeme ili kufanikisha utendakazi wake na hili hupandisha gharama ya kuvitumia kwa juu sana. Vilevile, mashine na vyombo vingi vya kielektroniki huhitaji ukarabati wa mara kwa mara ili kuviweka imara katika shughuli na kazi za utafiti kuhifadhi data kwa jumla. Mfumo wa utandawazi pia umesababisha uvumbuzi wa vifaa vingi vya kisasa na kufanya baadhi ya vifaa vya zamani kukosa matumizi yanayohitajika kwa kuwa na mitindo ya kizamani inayoendana na usasa. Hili basi husababisha mahitaji ya ghafla ya kuimarisha vifaa

hivyo vya zamani au hata kuviweka pembeni na kusababisha haja ya kununua vifaa vya kisasa vinavyoendana na mifumo ya utandawazi (Matundra, 2019). Mabadiliko kama haya ni ya lazima na kwa hivyo kuufanya mchangato mzima wa kuhifadhi lugha ya Kiswahili kuwa mgumu kwa jumla kutokana na mabadiliko hayo kama zao la utandawazi. Si siri, ni wazi kama meno ya ngiri kuwa utandawazi umepunguza shughuli za usafiri wa ana kwa ana, shughuli ya utafiti na kuhifadhi kwa data lazima usafiri uhusishwe kwa kutumia vyombo vya usafiri wa kisasa amabavyo pia ni zao la utandawazi. Usafiri wa kisasa ni wa gharama ya juu ikilinganishwa na awali kabla ya utandawazi kuchukuwa nafasi pana katika Maisha ya walimwengu (Massamba, 2002). Gharama hii ya juu na upungufu wa rasimali huishia kuwa changamoto kubwa katika uhifadhi wa lugha ya Kiswahili.

Mabadiliko ya Tamaduni:

Utamaduni huhusisha njia za maisha ya binadamu zinzojumuisha imani, sanaa, na taasisi ambazo zimekuwepo na zimefanywa kuwa sehemu ya maisha ya wanadamu husika. Kila jamii au eneo lina tamaduni zake ambazo huujenga mtindo wa jamii husika kutekeleza mambo yake na kufanya kuwa mtindo wao wa maisha. Mabadiliko katika tamaduni mbalimbali yameathiri pakubwa uhifadhi wa lugha ya Kiswahili kupitia njia ainati (UNESCO, 2010). Kwanza, njia ya asilia ambayo waja wengi walizoea kuhifadhi mambo na kuweka akilini ilikuwa kupitia akili zao amabazo kuhifadhi kumbukumbu hizo. Jamii nyingi zimebadili tamaduni kutokana na mfumo wa utandawazi ambapo kwa mfano mafundisho ya kale kutoka kwa wazee kuelekea kwa vijana au nyakanga kuelekea kwa mabanati waliofikia umri wa kuingia utu uzima yalititishwa kwa njia ya midomo na lugha ya kiswahili imekuwa nyenzo murua ya kupitisha maadili hayo. Tamaduni kama hizi zilisaidia pakubwa uhifadhi na kuhakikisha makuzi ya lugha ya Kiswahili kwa ujumla. Kutokana na utandawazi, mabadiliko mbalimbali yameshuhudiwa na hata kuibadili mitindo ya tamaduni hizo kupisha mitindo ya kisasa ya kuelimisha vijana kwa kutumia elimu ya kisasa. Elimu ya kisasa nayo kwa upande mwingine imebadili tamaduni hiyo ya kuitegemea lugha ya Kiswahili kama mojawapo ya lugha kongwe na kuhamia lugha zingine kama vile Kiingereza, Kifaransa, Kigiriki na Kilatino (Matundra, 2019). Jambo hili limeinyima lugha ya Kiswahili nafasi faafu ya kusambaa na kuhifadhiwa miongoni mwa wzungumzaji wake asilia.

Pili, utandawazi umechangia mabadiliko makubwa katika mitindo ya mawasiliano. Awali, tamaduni nyingi zilithamini mawasiliano ya ana kwa ana. Ujio wa a teknolojia ya kisasa na mfumo wa utandawazi umebadili mawasiliano baina ya waja ambapo vyombo vya kisasa vimeegemea pakubwa ili kurahisisha mawasiliano. Wingi wa mitambo ya kiteknolojia na vifaa vya kielektroniki vinavyotumika katika mawasiliano vimezipa lugha zingine kipaumbele ikilinganishwa na lugha ya Kiswahili. Hili jambo limechangia kudidimia kwa lugha ya Kiswahili na kuipa nafasi finyu katika mawasiliano. Vifaa hivi ibuka vinasababisha kuwepo kwa utandawazi unaojengeka kutokana na teknolojia ya kisasa. Hivi basi, vinainyima lugha ya Kiswahili nafasi ya kuenea kwa sababu lugha zingine kama vile Kiingereza zimepewa nafasi pana katika vifaa hivyo ili kutumika katika mawasiliano. Hili jambo linafanya uhifadhi wa lugha ya Kiswahili kukumbwa na changamoto kwa vile vifaa hivyo ndivyo nafasi murua ya kutekeleza uhifadhi huo ilhali vimetawaliwa na lugha zingine zinazoendana na mabadiliko ya utamaduni.

Tatu, tamaduni zimebadilika sana kutokana na kuongezeka kwa idadi ya watu duniani. Watu wengi duniani wameishia kuhamia kutoka makazi yao asilia na kuhamia sehemu tofauti duniani ili kufanikisha kusonga mbele na kuimarisha kwa mitindo yao ya maisha kwa msukumo wa utandawazi. Waja wengi wanapobadili makazi na mazingira na hata wengine kuhamia sehemu za kigeni, huishia kubadili tamaduni zao kwa sana na hata kuziacha lugha zao asilia. Kwa mfano, lugha ya Kiswahili imekuwa na kuenea kwa upana katika bara la Afrika kilinganishwa na mabara mengine duniani. Watu kutoka janibu za Afrika wanapohamia au kuzuri=u sehemu zingine kwa shughuli mbalimbali kama vile kiuchumi, kielimu na kidini, husababisha kubadili tamaduni zao ikiwemo lugha wanazozingumza kama vile lugha ya Kiswahili na kutwaa tamaduni za kigeni (Ndung'u na wenzake 2022). Hili huwafanya kushabikia tamaduni za ugenini pamoja na lugha za kigeni na kwa hivyo kufanya lugha ya Kiswahili kukosa nafasi murua kama tamaduni yao ya nyumbani. Watu kama hao husababisha kupunguka kwa idadi ya wazungumzaji wa lugha ya

Kiswahili na vilevile kutatiza shughuli za uhifadhi wa lugha yenyewe.

Sera Mbovu za Elimu:

Elimu pamoja na taasisi za elimu zimesalia kuwa kileleni katika kufanikisha shughuli za makuzi, maenezi na uhifadhi wa lugha mbalimbali ikiwemo lugha ya Kiswahili. Kufanikisha suala hili kumetokana na mitindo mipya ya kiteknolojia ambayo imechangia kuwepo kwa utandawazi. Hata hivyo, zama hizi za utandawazi zimechangia mabadiliko makubwa katika sekta ya elimu, kusababisha sera na mifumo mibaya katika elimu amabayo inazua changamoto katika uhifadhi wa lugha ya Kiswahili. Kwanza, taasisi nyingi za elimu zimezipa lugha zingine nafasi pana katika usomaji na fundishaji wa masomo mengi. Nchi kama vile Kenya, Nijeri, na Uganda katika bara la Afrika zimebuni sera amabazo zimetenga masomo yote kusomwa, kufundishwa na kuendeshwa katika lugha ya Kiingereza na lugha zingine za kigeni isipokuwa somo la Kiswahili. Hili suala hunyima Kiswahili nafasi sawa na lugha zingine. Vitabu vingi vya masomo tofauti kama vile uhandisi, uchongaji, ususi, ukulima, ubaharia, uanahabari, uanasaikolojia, utabibu, urubani na ufundishaji huandikwa katika lugha ya Kiingereza na kwa hivyo lugha hiyo kutumiwa kama hifadhi ya matini kwa masomo hayo. Somo la Kiswahili ndilo somo pekee ambalo huweza kuhifadhi matini yake kwa kutumia lugha iyio hiyo ya Kiswahili, kwa hivyo kuwa changamoto kwa lugha ya Kiswahili kuhifadhiwa kwa kuwa Kiingereza na lugha zingine zimechukuwa sehemu upan wa kuhifadhi maandishi vitabuni.

Sera nyingi za baadhi ya shule miongoni mwa mataifa haswa ya bara la Afrika pia zimejikita katika lugha za kigeni huku Kiswahili kama mojawapo ya lugha asilia ikitupwa katika kapu la saha. Kwa mfano, sheria na kanuni za taasisi za elimu zimeandikwa katika lugha ya Kimombo, Kiarabu, au hata Kifaransa na kushinikiza wanafunzi wote kuzikkariri na kuzifuata kwa masharti. Kwa kawaida sheria katika taasisi yoyote ile huwa ni kiungo na kifaa kinachoweleta watu pamoja na hutumika na taasisi hiyo kwa shughuli za kila siku. Sheria kama hizo zandikwapo katika lugha zingine bila kuzingatia lugha ya Kiswahili, uhifadhi, maendeleo na makuzi yake huegemea tu lugha zingine na kupipa Kiswahili nafasi finyu ya kushiriki katika uhifadhi huo. Hili hujitokeza kama changamoto kubwa katika uhifadhi wa lugha ya Kiswahili.

Sera zingine za elimu kama vile matangazo kwa wafanyakazi pamoja na wanafunzi kutoka kwa wakuu wao hupendelewa kuwasilishwa katika lugha zingine kando na lugha ya Kiswahili katika mikusanyiko ya taasisi za elimu kama vile gwaride na katika mikutano. Wahusika wengi wapewapo nafasi mbele ya hadhira yao kutekeleza shughuli kama vile kupiga dua kabla ya shughuli za shule hupendelea kutumia lugha za kigeni kama vile Kiingereza na Kiarabu. Lugha hizo hutumika kwa sana katika kufanya ibada za maombi na hata kusoma maandiko katika vitabu vya kidini. Hili huzua ushindani mkali baina ya lugha ya Kiswahili na lugha zingine. Uzoefu wa lugha zingine hufanya Kiswahili kuzewa kwa kiwango kikubwa, hivyo basi kupata nafasi ndogo sana ya kuhifadhiwa kwa sababu matumizi yake ni haba. Kwingineko, sera za elimu huagiza uajiri wa walimu wengi wa lugha zingine na masomo yasiyotumia lugha ya Kiswahili kuliko walimu wa Kiswahili kwa kigezo kuwa Kiswahili hutumika tu katika ufundishaji wa somo la Kiswahili pekee na kwa hivyo utendakazi wake ni mdogo sana. Idadi ya walimu wa Kiswahili katika taasisi hizi za elimu huwa finyu sana kwa hivyo kushusha iadadi maalum inayostahili katika kuendelea na kuhifadhi lugha hiyo.

Sheria zingine katika taasisi za elimu huwanyima wanafunzi uhuru wa kutumia lugha ya Kiswahili sawa na lugha zingine. Kwa mfano, baadhi ya sheria katika shule nyingi barani Afrika zimetenga siku chache mno za kuwaruhusu wanafunzi kutumia lugha ya Kiswahili ikilinganishwa na lugha zingine. Hili hufanya watafiti wengi katika zama za utandawazi kukosa hamu ya kufanya utafiti na kuhifadhi lugha ya Kiswahili katika viwango mbalimbali vya elimu kwa sababu Kiswahili kimepewa nafasi ndogo na kuonelewa kwamba hakihitaji utafiti wa kina na kuhifadhiwa (Ndung'u na wenzake, 2022). Baadhi ya kanuni za shule huelekeza wahusika kutoa adhabu kali kwa wanafunzi amabao huvunja kanuni za shule ikiwemo sheria ya kuzingatia sera za lugha. Kwa hivyo wanafunzi watumiaapo lugha ya Kiswahili kinyume na sheria na huishia kupewa adhabu kali na kuwafanya kuepuka lugha ya Kiswahili hivi basi kukosa kuizingatia na kuhifadhi kama lugha mojawapo ya mawasiliano.

Kukosekana kwa Uhamasishaji:

Uhamasishaji ni njia murua ya kushawishi na kushinikiza uzingatifu wa jambo lolote ambalo lipo katika hatari ya kuponyoka au kudidimia miongoni mwa waja katika jamii. Zama za utandawazi zina nafasi pana ya kuendeleza uhamasishaji kuhusu masuala kama hayo katika jamii. Ajabu ni kwamba zimeshuhudiwa kampeni chache mno za ana kwa ana na katika kurasa za mitandao kama vile Facebook, Twitter, Telegram, na Instagram zinazoshinikiza matumizi na uhifadhi wa lugha ya Kiswahili. Makundi mengi yanayoshuhudiwa katika kurasa hizi yanahusu lugha zingine kwa upana ikilinganishwa na lugha ya Kiswahili. Aidha, mabango mengi ya matangazo huwekwa katika lugha za Kiingereza na lugha zingine kama vile Kiarabu na Kifaransa bila kuzingatia uwepo wa lugha ya Kiswahili. Licha ya hayo, mabango machache sana hushabikia lugha ya Kiswahili kama kielelezo cha kukuza umoja kupitia mawasiliano kama chombo maridhawa cha kuleta watu pamoja (Ndung'u na wenzake, 2022). Suala hili hukosesha lugha ya Kiswahili nafasi nzuri ya kuhifadhiwa na kutumika kama lugha miongoni mwa makundi mbalimbali ya watu katika jamii. Uchache wa wazungumzaji katika lugha ya Kiswahili vilevile husababisha idadi ndogo ya watafiti na wahamasishaji wa lugha hii miongoni mwa mataifa ya ndani na nje ya Afrika na kwa hivyo kuifanya lugha ya Kiswahili kukosa mvuto ufaao. Kutamauka kwa watafiti na wahamasishaji wa lugha ya Kiswahili huwafanya wakose hamu ya kukipandisha Kiswahili hadhi faafu na hata kukosa sababu ya kuhifadhi kama lugha inayohitaji malezi na makuzi yafaayo. Juhudi za watu wachache ambao hujizatiti kufanya uhamasishaji kwa umma kuhusu namna ya kuendeleza, kukuza na kuhifadhi lugha ya Kiswahili pia hukumbwa na changamoto si haba (Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA), 2018). Mathalani, utafiti mwingi umebaini kwamba ujumbe wa kuhamsisha umma kuhusu uhifadhi na usambaaji wa lugha ya Kiswahili hufikia idadi ndogo sana ya waja. Hii imesababishwa na mifumo ya teknolojia na utandawazi kwa vile wataalamu wa lugha ya Kiswahili huchagua mitandao kuwa njia murua uya kupasha ujumbe kwa watu. Kinaya ni kwamba idadi ya watu wanaozuru kurasa mbalimbali za mitandao ni ya chini sana na kwa hivyo kuwa changamoto katika uhifadhi wa lugha ya Kiswahili.

Mabadiliko ya Teknolojia:

Cha kudumu duniani ni mabadiliko. Mifumo ya teknolojia ni mojawapo ya sehemu ya maisha ya binadamu ambayo imekumbwa na mabadiliko makubwa na ya mara kwa mara. Inaaminika kwamba mabadiliko haya hunuia kuimarisha na kurahisisha maisha ya binadamu ikilinganishwa na siku za awali Mitambo ya teknolojia kama vile tarakilishi hutumika kuhifadhi data muhimu zilizokusanywa na watafiti kuhusu Kiswahili. Uimarishaji na uvumbuzi wa mitambo ya kisasa mara nyingi haiendani na data za awali katika mita5mbo hiyo, na kwa hivyo kusababisha kupotea kwa data hiyo iliyohifadhiwa awali. Uhifadhi wa lugha ya Kiswahili pia hubainika kuwa mgumu ikilinganishwa na lugha nyingine katika zama za utandawazi. Hii inatoka na mitambo na vifaa vya kielektroniki kama vile tarakilishi amabazo hazijaratiwa kutambua lugha ya Kiswahili na kwa hivyo basi kufanya ukusanyaji na uhifadhi wa data kuhusu lugha ya Kiswahili kupata changamoto. Baadhi ya njia za kuhifadhi data kama vile kupiga picha na kupiga chapa nakala zinazohusu lugha ya Kiswahili pia zimekumbwa na maotatizo kama vile nakala zilizohifadhiwa hukaa muda na kupoteza uasili wake (Rubagumya, 2003). Baadhi ya picha za zamani zilizohifadhiwa pia hupitwa na wakati na kuzifanya zikose kazi katika mahitaji na mitindo mipya itokanayo na utandawazi. Kwa hivyo, maendeleo na mabadiliko ya kiteknolojia husalia kuwa changamoto katika uhifadhi wa data kuhusu lugha ya Kiswahili.

Uchache wa Watafiti:

Lugha ya Kiswahili ni lugha amabayo imebainika wazi kuwa na wazungumzaji wachache ikilinganishwa na lugha zingine duniani. Idadi ndogo ya wazungumzaji wa lugha hii vilevile huwa ni chanzo cha idadi ya chini ya watafiti. Utafiti ni shughuli pana ambayo huhitaji vifaa vya kutosha na wahusika waliohitimu katika sekta hiyo. Lugha zingine kama vile Kiingereza, Kiarabu, na Kifaransa zimefanyiwa utafiti wa kina kwa sababu watafiti wengi wamejihusisha na lugha hizo (East African Community (EAC), (2020). Kwa upande mwingine, lugha ya Kiswahili imeonelewa na watu wengi kama lugha ya hadhi ya chini na kwa hivyo kuifanya kuwa na wataalamu wachahe mno wanaokubali kujihusisha nayo. Vifaa kama vile vitabu vya utafiti na mitambo ya kisasa iliyo na data kuhusu lugha ya Kiswahili ina bei ghali sana. Bei za juu huwaogopesha wengi wa watafiti kuwafanya

kuepuka utafiti wa lugha ya Kiswahili na badala yake kujikita katika utafiti wa nyanja zingine za kitaaluma.

Lugha ya Kiswahili pia ina historia ndefu amabayo utafiti wake unapaswa kuhusisha wakongwe kama vifani wa kupeana ujumbe kwa watafiti nyanjani. Hili linakuwa gumu kwa vile wengi wa wazee wanaohusika na ujumbe kuhusu lugha ya Kiswahili maeneo mbalimbali wamefariki, kwa hivyo kupunguza idadi ya wahusika mahususi wanaopaswa kufanikisha uhifadhi wa lugha ya Kiswahili (Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili - Chuo Kikuu cha Dar es Salaam). Taasisi za elimu ya juu zinazofundisha lugha ya Kiswahili katika mataifa mengi duniani ni chache sana Afrika na duniani kwa ujumla. Kwa hivyo changamoto hii husababisha kuhitimu kwa wataalamu wa lugha ya Kiswahili kwa idadi ndogo sana. Hii ndiyo sababu ya kuwepo kwa idadi ndogo ya watafiti katika lugha ya Kiswahili na kwa hivyo kuwa tatizo katika utafiti na kuhifadhi kwa lugha ya Kiswahili.

Mitazamo Hasi ya Jamii Mbalimbali:

Kila jamii ina mitazamo yake kuhusu lugha zinazozungumzwa katika jamii hizo zikiwemo lugha asilia pamoja na zile za kigeni. Jamii nyingi ndani na nje ya bara la Afrika hushikilia kwamba mwanajamii kindakindaki anapaswa kuzingatia na kuionea fahari lugha yake ya kwanza kama thibitisho la kuzizingatia na kuziheshimu mila na desturi za jamii husika. Jamii ambazo Kiswahili si lugha yao ya kwanza basi hujikita katika lugha za kiasili na kuzitumia kwa upana kufanya lugha ya Kiswahili kukosa nafasi ya kutosha katika mazungumzo na kwa hivyo kufanya uhifadhi wake kuwa mgumu. Jamii za wanachuoni mbalimbali pia zina mitazamo tofauti kuhusu chimbuko na asili ya lugha ya Kiswahili. Wapo wanaoshikilia kwamba Kiswahili ni lugha ambayo asili yake ni kutokana na lugha za Kinbantu huku wakithibitisha kupitia mifanano ya miundo ya maneno na baadhi ya sauti katika matamshi. Mitazamo ya jamii zingine za wasomi na watafiti nao wanazingatia Kiswahili kuwa lugha ya asili ya Kiarabu kwa kigezo cha mfanano wa maneno ya Kiswahili na Kiarabu kwa upana (Matundra, 2019). Kwingine zipo jamii za wasomi zinaonelea kwamba Kiswahili ni lugha iliyobuniwa kutokana na mesto wa lugha tofauti tofauti kwa kukopa misamiti kutoka lugha hizo moja kwa moja kisha kukijenga Kiswahili. Mivutano hii kuhusu asili na chimbuko la Kiswahili huzua utata kuhusu ujumbe unaostahili kuhifadhiwa na kuaminiwa kama ujumbe sahihi kwa hivyo kuleta ugumu katika uhifadhi wa data aminifu kuhusu lugha hii. Jamii za kidini vilevile huleta mtafaruku kuhusu lugha ya Kiswahili, uasili wake pamoja na matumizi miongoni mwa waumini wa dini mbalimbali. Mathalani, zipo imani kwamba Kiswahili ni lugha yenye asili ya Kiarabu na ujio wake unambatanishwa na dini ya Kiislamu kwa kiwango kikubwa. Watu kutoka katika dini tofauti basi huibezwa lugha hiyo kwa kuamini kwamba sio lugha faafu katika kutumia na kuendeleza masuala ya dini zao. Watu kama hao wenye Imani kinzani kuhusu lugha ya Kiswahili basi huipa mgongo na kuegemea lugha zinh=gine kama vile Kiingereza n

Hamahama za Watu

Hamahama za watu husababishwa na shughuli mbalimbali kama vile utafutaji wa ajira, shughuli za masomo, shughuli za kiuchumi kama vile biashara, mabadilisho ya mazingira, majanga kama vile mafuriko, baa la njaa, sababu za kisiasa na uvamizi wa kibinadamu. Wakati mwingine hamahama zinaweza kujitokeza kama shinikizo la sheria kutoka katika serikali. Kutokana na kuhama kwa waja, tatizo la mabadiliko katika lugha hujitokeza miongoni mwa watu waliohusika katika hamahama hizo. Kwa mfano, watu waliohamia katika janibu tofauti huishia kuacha lugha yao pamoja na mila na desturi zao kisha kuchukua mitindo mipya pamoja na lugha za kigeni kwa kukopa kwa wenyeji wao. Wenyeji wa lugha ya Kiswahili wanapojikuta katika hali kama hii, husababisha wao kuchanganya lugha na hata na kufanya lugha ya Kiswahili kukosa mashiko yake asilia (Ndung'u na wenzake, 2022). Kwa hivyo ukusanyaji wa data kuhusu lugha ya Kiswahili na matumizi yake hupoteza uasilia ufaao na kufanya lugha inayohifadhiwa kama lugha ya Kiswahili kupoteza mkao na muundo wake kamili.

Suluhu na Mapendekezo:

Wanaisimu na watafiti wengi katika sekta za kielimu na kiakololojia wametoa mapendekezo ainati kama njia ya kutatua shida zinazokumba ukusanyaji na uhifadhi wa lugha ya Kiswahili. Watafiti mbalimbali wameangazia suluhu amabazo zimeangaziwa na baadhi ya mashirika ya kutetea na kukikiza Kiswahili (Baraza la Kiswahili la Taifa

(BAKITA). Hali kadhalika, watetezi wa kibinafsi pia wametoea suluhu na mapendekezo kadha wa kadha kama suluhu madhubuti kwa changamoto za kuhifadhi lugha ya Kiswahili. Kwanza, mashirika ya kutunza lugha ya Kiswahili yameshinikiza kuwepo kwa matumizi ya Kiswahili katika maeneo mbalimbali. Kuhimiza matumizi ya lugha yoyote katika maeneo mengi huipa lugha hiyo uwezo wa kupanua matumizi yake kwa sababu lugha hiyo hukubaliwa na kutumika katika sekta mbalimbali zikiwemo shughuli za kisisa, kisayansi, kitamaduni na kiuchumi.

Pili, kushinikiza kuwepo kwa matumizi ya lugha ya Kiswahili katika vyombo vya habari kama vile magazeti, redio, televisheni na majarida ni jambo adimu kama mojawapo ya harakati za kukuza, kuendeleza na kuhifadhi lugha ya Kiswahili. Vyombo vya habari vinafanikisha kupitisha lugha na kuenza matumizi ya lugha ya Kiswahili kwa idadi kubwa ya watu na kwa muda mfupi (UNESCO Digital Library - Reports on Language Sustainability). Hili litawezesha kuhifadhi na kukuza lugha ya Kiswahili kwa kitengo kipana. Kutafsiri nyaraka kadha wa kadha pia ni njia mojawapo ya kukuza na kuhifadhi lugha ya Kiswahili. Kiswahili kama mojawapo ya lugha kuu katika baadhi ya mataifa yakiwemo Tanzania na Kenya, utafsiri wa nyaraka muhimu za kitaifa husaidia katika uhifadhi na ukuzi wa lugha ya Kiswahili. Aidha, shughuli kama ukalimani zinapaswa kuwekwa kama mojawapo ya masomo shuleni ili kusaidia kuendeleza, kukuza na kuhifadhi lugha ya Kiswahili. Kuimarisha kwa masomo na kuajiri walimu zaidi wa somo la Kiswahili kutasaidia kuongezeka kwa idadi kubwa ya wanohitimu na kusaidia kuwepo kwa watafiti mashuhuri wa lugha ya Kiswahili. Kubadili mifumo mipya ya teknolojia na kubuni mitambo iliyoratibiwa ipasavyo ili kumudu kutambua lugha ya Kiswahili ili kusaidia kuikuza na kuhifadhi (Ndung'u na wenzake, 2022). Sera za elimu pia zinapaswa kufanyiwa marekebisho ili kukipa Kiswahili nafasi sawa na lugha zingine kama vile Kiingereza, Kifaransa na Kiarabu. kwingineko, serikali inapaswa kutenga rasimali ipasavyo ili vitengo kama vile taasisi zinazoshughulikia uchunguzi na uhifadhi wa lugha mbalimbali ikiwemo lugha ya Kiswahili zipate wakati mwepesi wa kutekeleza majukumu hayo.

Hitimisho:

Changamoto nyingi zinazohusishwa na uhifadhi wa lugha ya Kiswahili ni zao la utandawazi. Licha ya manufaa lufufu yanayohusishwa na utandawazi, zipo changamoto tele amabazo zimelemaza shughuli za uhifadhi wa lugha ya Kiswahili kutokana na mabadiliko na kuimarika kwa mifumo mipya ya teknolojia. Miongoni mwa hizi changamoto ni ushindani kati ya lugha ya Kiswahili na lugha nyingine za kigeni, sera mbovu za elimu, mabadiliko ya tamaduni za jamii mbalimbali nje na ndani ya bara la Afrika, upungufu wa watafiti, uchechefe wa pesa na rasimali zinazohitajika katika kuhifadhi lugha ya Kiswahili, hamahama za watu pamoja na mitazamo hasi katika jamii mbalimbali kuhusu lugha ya Kiswahili. Matatizo haya yanayokumba uhifadhi wa lugha ya Kiswahili yanaweza kutatuliwa kwa wepesi kuu ushirikiano baina ya serikali za nchi mbalimbali, taasisi za elimu na mashirika yaliyobuniwa sehemu mbalimbali duniani ili kussaidia kuhifadhi lugha ya Kiswahili. Miongoni mwa hizi suluhu ni uajiri wa walimu zaidi wa somo la Kiswahili, uboreshaji wa sera za elimu ili kukidhi mahitaji ya makuzi ya lugha ya Kiswahili, urekebishaji wa mitambo na mifumo ya teknolojia, uhamasishaji kuhusu somo la Kiswahili kwa kupitia vyombo vya habari pamoja na na kushinikiza na kufadhi mashirika mbalimbali yanayojihusisha na uchunguzi, ukusanyaji na uhifadhi wa lugha ya Kiswahili. Kwa hivyo, ni wajibu wa serikali zote pamoja na mashirika na taasisi za elimu kujumuika na kuweka mikakati ya kuhifadhi lugha ya Kiswahili kwani hii ndiyo mojawapo ya njia murua za kukukuza na kukiendeleza Kiswahili kama mojawapo ya lugha ambazo zimo katika hatari ya kudidimia.

Marejeleo:

- Abdulaziz, M. H. (1989). Factors Affecting the Development of Kiswahili as a National and International Language. *Kiswahili Journal*, Vol. 56.
- Anyonje, M. F., & Lihanda, M. K. (2024). Teknolojia ibuka na ufundishaji wa somo la Kiswahili. *East Africa journal of Kiswahili*, 3(1), 25-32. <https://doi.org/10.51317/eajk.v3i1.487>
- Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) (2018). Ripoti ya Hali ya Kiswahili Tanzania.
- Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA): www.bakita.go.tz
- Batibo, H. M. (2005). Language Decline and Death in Africa: Causes,

Consequences, and Challenges. *Multilingual Matters*.

East African Community (EAC), (2020). Policy on Kiswahili as an Official Language in the East African Region.

Kamau (2005) Matumizi ya Kiswahili katika tarakilishi chuo kikuu cha Kenyatta.

Kamusi ya Kiswahili Snifu. (2018) Tuki, Toleo la 4

Kihore, M. (2002). Kiswahili na teknolojia ya habari katika Mulika

Kioko, A. (2013). Language Planning and Policy in East Africa: Challenges and Opportunities.

Makala za Kisayansi

Massamba, D. P. B. (2002). Mchango wa Kiswahili katika Utandawazi: Changamoto na Fursa. Jarida la Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Matundura, B. (2019). KAULI YA MATUNDURA: Athari ya lugha za kigeni kwa Kiswahili. Taifa Leo. <https://taifaleo.nation.co.ke/makala/kauli-ya-matundura-athari-ya-lugha-za-kigeni-kwa-kiswahili/k>

Mazrui, A. & Mazrui, A. M. (1995). Swahili State and Society: The Political Economy of an African Language. East African Educational Publishers.

Mohochi, E (2002). Teknolojia ya mawasiliano na Nafasi Ulimwenguni katika utafiti wa Kiswahili, I.K

simala (Mhariri). Maseno: Chuo kikuu Cha Maseno

Mulokozi, M. M. (2004). Hali ya Kiswahili na Mustakabali Wake.

Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Munyakyiire, R(2021). Dhima ya teknolojia katika ujifunzaji na ufundishaji wa lugha ya Kiswahili. Chuo kikuu Cha Makerere

Ndung'u, P. M., Gacheiya, R. M., na Kitetu, C. W. (2022). Mitazamo ya Lugha na Utambulisho wa Kijamii Miongoni mwa Wazungumzaji wa Kindia na Kĩgĩchũgũ. *East African Journal of Swahili Studies*, 5(1). <https://journals.eanso.org/index.php/eajss/article/view/769/1180>

Ripoti na Nyaraka Rasmi

Rubagumya, C. M. (2003). Language Promotion for Educational Purposes: The Example of Kiswahili in Tanzania.

Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili - Chuo Kikuu cha Dar es Salaam: www.tuk.ac.tz

UNESCO (2010). Language Vitality and Endangerment: Documenting and Sustaining Endangered Languages.

UNESCO Digital Library - Reports on Language Sustainability: <https://unesdoc.unesco.org>